LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Block 44, Plot 508 & 509, Kijitonyama,
P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA • Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037,
E-mail: lhrc@humanrights.or.tz Website: www.humanrights.or.tz

for a Just and Equitable Society

19 Machi 2015

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI JUU YA MWENENDO NA HATUA ZA KISHERIA KWA VIONGOZI WA UMMA WANAOKIUKA MAADILI.

Ndugu WanaHabari,

Moja ya kazi za **Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu** ni pamoja na kufuatilia shughuli za Serikali kwa lengo la kuona inavyotimiza wajibu wake kwa wananchi.

Katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara ya 132 ibara ndogo ya (1) (5) imeunda Sekretarieti ya Maadili na Viongozi wa Umma. Pamoja na Katiba kuunda vyombo vya kusimamia maadili ya viongozi hali inaendela kuwa mbaya siku hadi siku, bado rushwa inaendelea kushamiri na matumizi mabaya ya rasilimali za umma na viongozi wameendelea kujipatia fedha kwa njia zisizo halali, bado kauli za kejeli na dharau zimeendelea kutolewa na viongozi, na zaidi ya yote hata mapendekezo yaliyowekwa katika rasimu ya pili ya katiba na Tume ya Kukusanya maoni juu ya maadili ya viongozi yalitolewa yote katika katiba pendekezwa.

Rushwa, matumizi mabaya ya rasilimali za umma na kujipatia fedha kwa njia zisizo halali,
Ndugu Wana habari,
Pamoja na kuwepo na Katiba na Sheria yenye muongozo juu ya maadili. Ndani ya muongo huu kumekuwa na matukio makubwa ya ukiukwaji wa maadili kwa viongozi wa umma ambapo viongozi wetu wamekuwa na matumizi mabaya ya rasilimali za umma pamoja na kujilimbikizia fedha na mali kinyume na sheria, ikiwemo rushwa, wizi na ubadhilifu, katika kipindi kisichozidi miaka 9 kumeripotiwa kashfa kubwa nne ambazo kwa ujumla wake zimeisababishia Taifa hasara ya zaidi ya shilingi bilioni 250. Ambapo kwa wastani inapoteza takribani asilimia 20% ya bajeti yake kila mwaka.

Mifano hii ni pamoja na mabilioni ya shilingi kupitia ununuzi wa rada iliyotumika kutoka Kampuni ya BAE Systems ya Uingereza, wizi wa mabilioni katika Akaunti ya Malipo ya Madeni ya Nje (EPA) ndani ya Benki Kuu (BoT), mkataba usio na tija kwa taifa na kampuni ya Richmond, kashfa ya mabilioni ya pesa waliyogaiwa viongozi wa juu na mfanya biashara kutoka kwenye akaunti ya Tegeta Escrow.

kauli za kejeli na dharau
Ndugu Wana habari,
Pamoja na kuwa na angalizo la kikatiba jitihada za Bunge kama mhimili wenye dhamana ya kuisimamia serikali zimekuwa zikikwamishwa na serikali. Mwenendo wa kuweka pingamizi Mahakama kuu na kuzuia baraza la maadili kufanya kazi yake kikatiba limeonesha mwanya na udhaifu wa Sheria na vyombo vya kusimamia maadili ya viongozi umma. Kwa kuwa sekretarieti

Board of Directors:
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), , Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

inaundwa kikatiba. Sekretariat inakazi, nguvu na mipaka yake na inatakiwa kutoingiliwa pale inapokuwa inashughulikia masuala ya kimaadili. Kwa mapingamizi yaliyowekwa na kusababisha baraza lisiendelee na kazi yake kama lilivyopanga inaonesha wazi ni jinsi gani vyombo vya kusimamia maadili ya viongozi zinavyopuuzwa.

Kauli za kejeli na za dharau kutoka kwa viongozi wetu, katika nyakati tofauti wamekuwa wakiendelea kuwakejeli wananchi kwa kauli hizo hata pale ambapo wananchi wanakuwa wamehoji mambo ya msingi. Hakuna hatua zozote zinazochukuliwa kwa viongozi wanaotoa kauli hizo ambazo ni kinyume kabisa na maadili ya uongozi wa umma, kauli hizo zimetolewa Bungeni, mara ingine kauli hizo zimetolewa kwenye vyombo vya habari na hata katika vyombo vinavyo simamia maadili ya viongozi wa Umma. Mifano yenyewe ni pamoja na;

- *"Sikumwomba James Rugemalira fedha. Na sijui kwa nini aliniwekea fedha hizo. Hata aliponiambia nifungue akaunti benki ya Mkombozi ili aniwekee fedha sikumwuliza fedha hizo ni za nini".*
- *"hiyo million 10 si pesa ya mboga tu"*
- *"nina account nyingi na za nje ya nchi kama ningetaka ningeweza kumwambia aziweke fedha akaunti za huko"*

Kauli hizo chache za kebehi na kejeli kutoka kwa viongozi wa umma wakati wa mwendelezo wa mashauri katika baraza la maadili zinaenda sambamba na kauli nyingine ambazo zilishawahi kusemwa huko nyuma kama;

- *'mtakula hata majani, lakini ndege ya raisi lazima inunuliwe'*
- *'Ili Serikali iachane na mpango huu, ni vema wale wote wanaopinga hatua hiyo kufanya hesabu za kiasi cha fedha kitakachopatikana kila mwaka katika kipindi chote cha mradi huo na kuilipa serikali'*
- *'hivi vijisenti tu'*
- *'Kama mtu hatoweza ongezeko la bei ya pantoni aogelee'*

Hizo ni baadhi tu ya kauli zilizowahi kutolewa na baadhi ya viongozi wetu ambazo dhahiri zinaonyesha kuwepo kwa kasoro kubwa katika swala zima la uongozi na uwajibikaji wa viongozi wetu. Mfumo wa nchi unaozalisha viongozi wawe wa kuchaguliwa au kuteuliwa.

Katika rasimu ya pili ya Katiba iliyopendekezwa na Tume ya mabadiliko ya Katiba chini ya Mh. Jaji Josseph Sinde Warioba katika sura ya Tatu (III): sehemu ya kwanza inayozungumzia maadili ya viongozi wa umma na sehemu ya pili inayozungumzia miiko ya viongozi wa Umma, sura hii ilikuwa imewasilishwa kwa uweledi wa hali ya juu na ilikuwa na ibara 10 (ya 13 hadi ya 22) zenye lengo la kuwabana na kuwawajibisha viongozi wa Umma. Na kwa bahati mbaya sana katika rasimu ya Katiba pendekezi wamezipunguza sura hizo kutoka 10 mpaka 4 pasipo kuwa na sababu yoyote ya msingi na ikumbuke kwamba katiba hii pendekezwa ndio iliandaliwa na viongozi hawa wenye kutokutaka kuwajibika.

Ndugu wanahabari,

Uwajibikaji wa viongozi kwenye taifa lolote ndio kiini cha kuwepo kwa maendelo ya kudumu na endelevu pia imani kwa wananchi. Viongozi ndio tunaowapa dhamana ya kupanga mipango ya maendeleo kwa kushirikiana na wananchi na yenye kugusa maslahi na maisha yetu ya kila siku,

Board of Directors:
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv, , Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

kututengenezea sheria na sera. Pia ndio wenye kuchangua na kutuidhinishia misaada na mikataba ya mikopo na deni la taifa. Hivyo ni muhimu kuwepo na sheria na vyombo imara vyenye kusimamia maadili na miendo yao kwa maendeleo yetu sote. Ni wazi kabisa wananchi wakikosa imani na viongozi wao ushirikiano wa kuleta maendeleo na hata amani hupungua.

Ndugu WanaHabari,
Baada ya kuona yote haya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapendekeza,

1. Viongozi wote wa heshimu Katiba ya Jamuhuri ya muungano wa Tanzania 1977 na Hususani Ibara ya 132 na nguvu na mamlaka ya sekretarieti ya maadili ya viongozi wa Umma kama ilivyoanishwa.
2. Sheria ya Maadili ya viongozi wa Umma itekelezwe kama ilivyoainishwa na Sekretariat ya maadili ya viongozi wa umma. Pia viongozi wawajibishwe kwa Kauli zao zeye kuonyesha dharau au kebehi kwa mifumo tulio jiwekea ituongoze, sheria au watanzania kwa ujumla.
3. Katiba iliyopendekezwa haijashinikiza uwepo wa uwajibikaji kwa viongozi wanao na watakao tuongoza na hivyo ni muhimu uwajibikaji uwepo kwenye katiba.
4. Watanzania wasome na wajihusishe kwenye mambo yanayo wagusa kama viongozi walio wachangua na kushinikiza uwajibikaji wao.
5. Wanahabari waendelee kuibua na kufuatilia maswala yenye kuonyesha uwajibikaji au kuto kuwajibika kwa viongozi wa umma na kushinikiza uwajibikaji wao.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

.....

Helen Kijo-Bisimba
Mkurugenzi Mtendaji
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

Board of Directors:
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.